

TUME YA NGUVU ZA ATOMIKI TANZANIA



03 April, 2018

TAARIFA KWA WADAU NA WATEJA WETU WOTE JUU YA MFUMO MPYA WA MALIPO

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) inawataarifu wadau na wateja wake wote kuwa kuanzia tarehe 03 Aprili 2018, Tume imehamia rasmi katika mfumo wa malipo wa Serikali wa "Government e-Payment Gateway- GePG)" kama matakwa ya kisheria kwa Taasisi zote za Serikali.

Tume ya Nguvu za Atomiki ni miongoni mwa Taasisi za Serikali ambayo imeanza kutumia mfumo huu kwa kufanya malipo kupitia Taasisi za kifedha ambazo zimejiunga na mfumo huu kama vile **MPESA, TIGOPESA, AIRTEL MONEY** na **NMB** Wakala.

Wateja wote mnatakiwa kuwa na namba maalumu (Control Number) ambayo inapatikana katika ofisi za Tume kwa ajiri ya malipo yote.

Tafadhari wasiliana na makao makuu ya Tume, Arusha. Pia na wahasibu katika ofisi za kanda za Dar-es-Salaam na Zanzibar.

Imetolewa na ofisi ya;

Mkurugenzi Mkuu
Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania
S.L.P 743,
Block J, Plot No 216, Njiro
Simu Na; +255 27 2970050/51/52/53
Arusha

Tanzania.